FRIEDRICH EBERT STIFTUNG

# Utaratibu wa Uteuzi wa Wagombea Ndani ya Vyama Tanzania

## Uchambuzi wa Kijinsia

www.fes-tanzania.org



www.fes-tanzania.org

# Utaratibu wa Uteuzi wa Wagombea Ndani ya Vyama Tanzania
# Uchambuzi wa Kijinsia

Julai 2020

Na Consolata Sulley
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

# Yaliyomo


Vifupisho 5

Shukrani 6

Utangulizi 7

Mbinu ya Utafiti 12

Mfumo wa sheria za nchi na mfumo wa kitaasisi 13

Kanuni za vyama na uwakilishi wa wanawake 18

Uchambuzi wa hali ya vyama vya siasa na uwakilishi wa wanawake 19

Sifa za kugombea 22

Kuchuja, kupiga kura na maamuzi ya mwisho 24

Hitimisho na mapendekezo 27

Marejeleo 31

Kiambatisho Na. 1: Watu walioshiriki 35

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| ACT-Wazalendo | Alliance for Change and Transparency |
| AZAKI | Asasi za Kiraia |
| BAWACHA | Baraza la Wanawake Chadema |
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| CHADEMA | Chama cha Demokrasia na Maendeleo |
| CUF | Civic United Front |
| FES | Friedrich Ebert Stiftung |
| IDEA | International Institute for Democracy and Electoral Assistance |
| IFES | International Foundation for Electoral Systems |
| NCCR-Mageuzi | National Convention for Construction and Reform |
| NDI | National Democratic Institute |
| NEC | National Electoral Commission |
| NEC | National Executive Committee |
| ORPP | Office of Registrar of Political Parties |
| TCD | Tanzania Centre for Democracy |
| TEMCO | Tanzania Election Monitoring Committee |
| TUCTA | Trade Union Congress of Tanzania |
| URT | United Republic of Tanzania |
| UWT | Umoja wa Wanawake Tanzania (CCM) |

# Shukrani

Utafiti huu usingeweza kukamilika bila ya msaada kutoka taasisi mbalimbali na watu binafsi. Kwakuwa si rahisi kuwataja wote hapa, ningependa kwa namna ya kipekee niishukuru taasisi ya Friedrich Ebert Stiftung (FES) ofisi ya Tanzania kwa kuniwezesha kifedha kufanya utafiti huu pamoja na kunipatia maoni mbalimbali. Napenda pia kumshukuru Bw. Issa Omary kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kunisaidia katika zoezi la ukusanyaji wa data.

Ningependa pia kwa namna ya kipekee kumshukuru Dkt Bashiru Ally, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Bw. Tumaini Makene, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Bi. Magdalena Sakaya (MB), Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF), Bw. Zitto Zuberi Kabwe, Kiongozi wa chama cha ACTWazalendo na Bi. Dorothy Semu, Makamu wa Mwenyekiti (Bara), chama cha ACTWazalendo. Napenda kuwashukuru si tu kwa kukubali kutoa maoni yao bali pia kwa msaada wao uliowezesha kufanyika kwa mahojiano na washirika wengine wa kutoka kwenye vyama vyao. Shukrani kama hizi nazitoa pia kwa maofisa wote wa vyama, wagombea wa uchaguzi uliopita, watia nia na wawakilishi wa Asasi za Kiraia (AZAKI) kwa kutoa maoni yao. Hata hivyo maoni yaliyoandikwa kwenye chapisho hili ni matokeo ya uchambuzi binafsi wa mwandishi ambaye anawajibika kwa mapungufu yoyote yatakayojitokeza.

# Utangulizi

Tafiti zinazohusu uwakilishi mdogo wa wanawake kwenye uongozi wa kisiasa katika bara la Afrika zimejikita zaidi kuangalia mifumo ya kisheria, aina ya mfumo wa uchaguzi, hali ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya nchi, na sababu za kiutamaduni (IFES, 2017; Stockemer, 2011; Norris, 2006; IDEA, 2005). Tafiti nyingine zimeangazia kuhusu ushindani kati ya vyama na vyama na kwa nini vyama vinashinda au kushindwa (Bratton & Van de Walle, 1997; Makulilo, 2007; Levitsky & Way, 2010; Raphael, 2010; Sulley, 2015a, 2015b; Tanzania Election Monitoring Committee (TEMCO), 1997, 2001, 2006, 2011, 2016). Tafiti hizi na nyingine nyingi hazijagusia mchango wa mchakato wa ndani ya vyama kama sababu inayochangia kuwepo na wanawake wachache kwenye nafasi za uongozi wa kisiasa. Kimsingi, siasa za ndani ya vyama na hasa uteuzi wa wagombea limekuwa ni jambo ambalo limefanyiwa utafiti zaidi katika nchi zilizoendelea kidemokrasia (Duverger, 1954; Gallagher, 1988, Hazan na Rahat, 2010; von Berge & Poguntke, 2017). Ni muhimu kufanya utafiti kuhusu mchakato wa ndani ya vyama kwasababu mchakato wa uteuzi unaathiri kwa kiasi kikubwa aina ya watunga sheria za nchi na sera wanazotunga (Gallagher and Marsh, 1988). Kuelezea kwa kifupi kuhusu umuhimu wa uteuzi wa wagombea, Schattschneider (alinukuliwa na Hazan & Rahat, 2010: 8) ambapo alisema:

*"…uteuzi wa wagombea ni zoezi muhimu sana kwa chama chochote kile. Umekuwa ni alama muhimu sana ya kuvipambanua vyama vya wakati wetu wa sasa. Kama chama hakiteui wagombea, kinapoteza sifa ya kuwa chama cha siasa. Aina ya mchakato wa kuwapata wagombea unaelezea jinsi chama cha kisiasa kilivyo. Yeyote mwenye mamlaka ya kuwateua wagombea ni mmiliki wa chama. Uteuzi wa wagombea ni kigezo muhimu sana cha kuangalia namna madaraka yanavyogawanywa ndani ya chama".*

Katika kutekeleza jukumu hili la kuwapata wagombea, vyama vya siasa barani Afrika kwa ujumla na hasa kwa namna ya pekee Tanzania vimekuwa vikiteua wanawake wachache kugombea nafasi mbalimbali. Kwa mfano, kati ya wagombea 14,501 walioshiriki kwenye uchaguzi wa mwaka 2017 nchini Kenya, wanawake walikuwa 1,259 (8.7%) (FIDA Kenya, 2018: 28). Kwa upande wa Afrika ya Kusini, kati ya wagombea 2,089 wa ubunge, wanawake walikuwa 827 (39.6%) (NEC South Africa, 2014: 27). Kwa upande wa Tanzania, kuna ushahidi wa kutosha kuwa uwakilishi wa wanawake kwenye uchaguzi ni mdogo. Kati ya wagombea 11,933 waliogombea nafasi mbalimbali kuanzia uraisi, ubunge na udiwani kwa uchaguzi wa mwaka 2015, wanawake walikuwa 904 tu (7.5%) (NEC, 2016: 43-45). Kwa hakika, asilimia ya wanawake wanaoshiriki kwenye siasa kuanzia kujiandikisha kupiga kura hadi kuomba nafasi za uwakilishi kwenye siasa inakuwa ikipungua. Wakati idadi ya wanawake waliojiandikisha kupiga kura mwaka 2015 ilikuwa asilimia 53 ya wapiga kura wote, ni asilimia 7.5 pekee ndio walioteuliwa kugombea nafasi mbalimbali, na waliopita kwenye uchaguzi walikuwa ni asilimia 5.4 pekee (NEC, 2016: 72-75). Jedwali namba 1 linaonesha asilimia za wabunge walioteuliwa na vyama vyote vilivyosajiliwa Tanzania tangu mwaka 2005. Hata kama hakuna ongezeko halisi tangu mwaka 2005, asilimia ya wagombea wanawake bado iko chini sana kufikia kuwa sawa na ya wanaume.

**Jedwali namba 1: Mchanganuo wa kijinsia wa wagombea ubunge waliopitishwa mwaka 2005, 2010 na 2015**

| MWAKA | WANAUME | WANAWAKE | JUMLA | % YA WANAWAKE |
|---|---|---|---|---|
| 2005 | 1,063 | 159 | 1,222 | 12.7 |
| 2010 | 845 | 191 | 1,036 | 18.4 |
| 2015 | 976 | 233 | 1209 | 19.2 |

Chanzo: Ripoti za Uchaguzi Mkuu Tanzania za Tume ya Taifa ya Uchaguzi za Mwaka 2005, 2010 na 2015

Hali hairidhishi tukiangalia teuzi za chama kimojakimoja na hali ni mbaya zaidi hasa kwa vyama ambavyo vina uwezo mkubwa wa kushinda uchaguzi. Vyama vikubwa1 kama Chama cha Mapinduzi (CCM) na kile cha upinzani Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) vimekuwa vikiteua wagombea wananwake wachache zaidi ukilinganisha na vyama vichanga.

**Jedwali 2. Wagombea Ubunge waliopitishwa na baadhi ya vyama mwaka 2015**

| CHAMA | WAGOMBEA | JINSIA | | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| | | ME | KE | %KE |
| ACT-W | 203 | 173 | 30 | 14.7 |
| CCM | 264 | 240 | 24 | 9 |
| CHADEMA | 184 | 171 | 13 | 7 |
| CUF | 135 | 120 | 15 | 11 |
| NCCR-M | 27 | 21 | 6 | 23 |

Chanzo: Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC 2016 uk. 46).

Ni vizuri kutambua kuwa, wanawake wanaopitishwa kugombea wanakuwa na nafasi kubwa ya kuibuka washindi kwenye uchaguzi. Uchambuzi wa masuala ya kijinsia kwenye uchaguzi wa Kenya wa mwaka 2017 unaonesha kuwa wanawake waliochaguliwa kugombea walishinda uchaguzi na hivyo idadi ya wanawake2 waliochaguliwa mwaka 2017 iliongezeka ukilinganisha na mwaka 2013. Gauja & Cross (2015) walibaini matokeo kama hayo kwenye utafiti wao waliofanya katika nchi ya Australia kwa kuangalia ushiriki wa wanawake kwenye uchaguzi. Walibaini kuwa, idadi kubwa ya wanawake waliopitishwa na vyama vyao kugombea walishinda uchaguzi na kuwa wabunge. Uchaguzi wa wabunge wa mwaka 2015 nchini Tanzania unaonesha kuwa wagombea ubunge wanawake 18 kati ya 24 wa CCM na wagombea ubunge wanawake 6 kati ya 13 wa CHADEMA3 walishinda kwenye uchaguzi. Wanawake hawa walioshinda ni sawa na asilimia 9 na 17 ya wabunge wote waliochaguliwa wa CCM na CHADEMA, mtawalia4. Katika chaguzi za huko nyuma, wagombea waliopitishwa na chama cha CCM walifanya vizuri zaidi. Mathalani mwaka 1995,5 CCM ilikuwa na wagombea wanawake 7 na wote walishinda. Mwaka 2000 wagombea wanawake wa CCM walikuwa 13 na kati ya hao wagombea 12 walishinda. Pia mwaka 2005 kulikuwa na wagombea wanawake 19 na kati ya hao 17 walishinda. Mwaka 2010 kulikuwa na wagombea 24 ambapo kati ya hao 19 walishinda (NEC 1996; 2001; 2006 & 2011).

Takwimu za hapo juu zinaonesha kuwa kadiri vyama vinavyowachagua wanawake wengi kugombea nafasi za uongozi kwenye chaguzi ndivyo vinavyokuwa na uwezekano mkubwa wa kuongeza idadi ya wanawake kwenye ngazi za uwakilishi kama vile bungeni. Kuhusu hili Gauja na Cross (2015) wanasisitiza kuwa, "kama wapiga kura hawana mtazamo hasi kuhusu wanawake wakati wa kupiga kura, basi ipo haja kwa vyama vya siasa kuruhusu wanawake wengi zaidi kugombea nafasi mbalimbali kwenye uchaguzi. Hii inamaanisha kuwa kuna haja ya kuwa na wanawake wengi zaidi kwenye akiba ya wagombea". Kwa kuzingatia umuhimu wa mchakato wa uteuzi wa wagombea katika kupata wawakilishi katika nafasi mbalimbali za dola, ni muhimu kuchambua taratibu za vyama mbalimbali za kuwapata wagombea na namna taratibu hizo zinavyoathiri usawa wa kijinsia na uwakilishi wa wanawake.

[1]Tunapima ukubwa au udogo wa chama kwa kuangalia kinavyopata mafanikio kwenye uchaguzi kwa kuangalia idadi ya kura na viti vya uwakilishi.

[2]Uchambuzi wa Kijinsia uliofanyika mwaka 2018 kuhusu Uchaguzi wa Kenya wa Mwaka 2017.

[3]Nusu ya wagombea wanawake kutoka CHADEMA walishindwa kwenye uchaguzi, ikiakisi taswira halisi ya mafanikio ya jumla ya chama kwenye uchaguzi 2015.

[4]Uwiano wa wagombea wanaume kwenye uchaguzi wa 2015 ni: CCM 240 na CHADEMA 171 kama inayooneshwa kwenye Jedwali la 2.

[5]Uchaguzi Mkuu wa kwanza wa vyama vingi uliofanyika Tanzania baada ya kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992

Tofauti na hali ya jumla iliyoelezwa hapo juu, utafiti huu unachambua kanuni na taratibu za kuwapata wagombea ndani ya vyama vya siasa vinne ambavyo vilichaguliwa makusudi. Vyama hivyo ni Chama cha Mapinduzi (CCM), Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Civic United Front (CUF) na Alliance for Change and Transparency (ACT-Wazalendo). Ziko sababu mbili zilizofanya vyama hivi vichaguliwe. Kwanza, kila chama kilikuwa na mgombea wa ubunge kwenye uchaguzi wa mwaka 2015. Pili, kama ambavyo takwimu za uchaguzi za mwaka 2015 zinavyoonesha, vyama hivi vilikuwa na wagombea kwenye zaidi ya nusu ya majimbo ya uchaguzi nchini Tanzania. Mbali na kuwa na wagombea wengi kwa zaidi ya nusu ya majimbo yote, ni jambo la kushangaza kuona kuwa idadi ya wanawake katika vyama hivyo ilikuwa ndogo kama ilivyooneshwa kwenye jedwali namba 2 hapo juu. Hivyo basi, malengo mahususi ya utafiti huu ni kutaka kujibu maswali yafuatayo.

1. Ni sheria zipi za kitaifa na mifumo ya kitaasisi inayopigania usawa wa kijinsia kwenye mchakato wa kuwapata wagombea na sheria zipi zinakwamisha usawa wa kijinsia?
2. Ni kwa namna gani vyama vya siasa vinawapata wagombea na ni kwa kiasi gani mchakato huo ni wa kidemokrasia na unajumuisha masuala ya kijinsia ?
3. Ni mambo gani yanahimiza/kukwamisha ushiriki wa wanawake na mafanikio yao katika kugombea nafasi za uwakilishi kupitia vyama vya siasa?

Utafiti huu umebaini kuwa vipo vifungu vya sheria ndani ya nchi vinavyosisitiza kuhusu usawa wa kijinsia na pia zipo kanuni za kuzuia ubaguzi wa kijinsia. Hata hivyo, kuna udhaifu katika kuvifanya vyama vya siasa kusimamia sheria na kanuni hizo kwa ajili ya kutetea demokrasia na usawa wa kijinsia kwenye michakato yao ya ndani. Ofisi ya msajili wa Vyama vya Siasa inayosimamia shughuli za vyama vya siasa ni dhaifu kimuundo na kirasilimali katika kusimamia matwakwa ya kisheria yanayovitaka vyama vya siasa kuzingatia demokrasia na usawa wa kijinsia.

Pia, vyama vimekuwa vikionesha kwenye katiba zao kuwa vinasimamia kanuni za usawa wa kijinsia bila kubagua watu kwa sabababu yoyote ile. Udhaifu mkubwa kwenye vyama hivyo vinne ni kuwa hakuna uhusiano kati ya kile kilichoandikwa kwenye katiba zao na kile kinachotekelezwa. Hakuna miongozo wala mifumo ya kusimamia vyama vya siasa ili viweze kuzingatia usawa wa kijinsia wakati wa kuteua wagombea. Zaidi ya hapo, vyama hivi vyote vinne vina mchakato wa uteuzi wa wagombea unaotoa mamlaka kwa wachache, usio na demokrasia na ambao kwa kiasi kikubwa unatawaliwa na wanaume. Hivyo basi, uteuzi wa wagombea wanawake unategemea kwa sehemu kubwa utashi wa vyombo vya maamuzi vya vyama badala ya kutegemea mifumo inayolenga kuleta usawa wa kijinsia katika mchakato wa uteuzi.

Mpangilio wa ripoti hii uko kama ifuatavyo: Sehemu ya kwanza ni utangulizi, ikifuatiwa na sehemu inyoongelea mbinu ya utafiti na ukusanyaji wa data. Sehemu ya tatu inafanya mapitio ya sheria za nchi na mifumo ya kitaasisi kutathmini kama sheria na mifumo hiyo inapigania usawa wa kijinsia au inakwamisha usawa wa kijinsia kwenye mchakato wa kuwapata wagombea ndani ya vyama. Sehemu ya nne ya ripoti hii inaangazia kanuni na taratibu za uteuzi wa wagombea ndani ya vyama, na namna kanuni na taratibu hizo zinavyoathiri uteuzi wa wanawake kwenye kugombea nafasi za uongozi wa kisiasa. Sehemu ya tano ya ripoti hii ni hitimisho na mapendekezo.

# Mbinu ya Utafiti

Utafiti huu ulitumia mbinu ya ufuatiliaji wa kina. Mbinu hii ilichaguliwa kwa lengo la kutaka kupata uelewa zaidi kuhusu mbinu zinazotumika kuwapata wagombea kwa mrengo wa kijinsia. Zaidi ya hayo, mbinu hii ya ufuatiliaji wa kina inawezesha ukusanyaji wa data kutoka vyanzo vya msingi na vyanzo vya ziada. Ukusanyaji wa data katika utafiti huu ulifanyika kwa kufanya mapitio ya nyaraka pamoja na kufanya mahojiano na wahusika mbalimbali. Kulifanyika mapitio ya mifumo ya kisheria, katiba za vyama, kanuni na taratibu kwa ajili ya kuchunguza kama zinakwamisha au kupigania usawa wa kijinsia katika mchakato wa uteuzi wagombea ndani ya vyama. Pia ripoti za uchaguzi, ripoti za uangalizi wa uchaguzi na za vyombo vya habari zilitumika kama vyanzo muhimu vya kusaidia kufanya tathmini ya namna vyama vya siasa vinaendesha mchakato wa kuwapata wagombea.

Zaidi ya hayo, mahojiano[6] yaliyowahusisha wadau muhimu yalifanyika. Wadau hao ni pamoja na viongozi wa vyama, wawakilishi wa jumuiya za wanawake ya vyama vya siasa, wagombea wa kipindi cha nyuma, watia nia wa chaguzi zilizopita, wagombea na wabunge. Hao wote walichaguliwa ili kujifunza kuhusu mchakato halisi wa kuwapata wagombea, hasa uzoefu wa wanawake wenyewe. Kundi jingine muhimu lilifanyiwa mahojiano ni Asasi za Kiraia (AZAKI) na vyama vya wafanyakazi. Mashirika mbalimbali yanayojihusisha na haki za wanawake na jinsia yalihusishwa pia. Mbali na hao wote, mamlaka inayosimamia uchaguzi, yaani Tume ya Uchaguzi (NEC) na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa nayo ilihusishwa. Tume ya Uchaguzi inahusika kusimamia uchaguzi wa kiushindani kati ya vyama mbalimbali vya kisiasa, ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa inasimamia ufanyaji kazi wa vyama hivyo pamoja na michakato yao ya ndani.

[6]Orodha ya walioshiriki kwenye mahojiano iko katika kiambatanisho namba 1.

# Mfumo wa kisheria wa nchi na wa kitaasisi

Vyama vya siasa ni taasisi zilizoanzishwa kisheria, vinafanya kazi kwa mujibu sheria na mifumo ya nchi. Ni jambo muhimu na la lazima kuangalia jinsi sheria za nchi na za taasisi zinavyosaidia au kukwamisha usawa wa kijinsia ndani ya vyama vya siasa wakati wa uteuzi wa wagombea. Sheria muhimu za nchi zinazosimamia shughuli za vyama vya siasa ni pamoja na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977; Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984; Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 (iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019; Sheria ya Uchaguzi Na. 1 (sura ya 343) ya mwaka 1985 na Kanuni za uchaguzi.

Utafiti ulibaini kuwa mfumo wa sheria wa nchi unasisitiza haki sawa kwa wote. Ibara za 12(1) (2) na 21 (1) (2) za Katiba ya Muungano na ile ya Zanzibar zinaeleza wazi kabisa kuwa binadamu wote ni sawa mbele ya sheria na kila mwananchi ana haki ya kushiriki katika masuala ya umma yakiwemo ya uongozi wa taifa. Sheria ya vyama vya siasa iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019 inajaribu kuzungumzia usawa wa kijinsia na uepukaji wa ubaguzi kwenye vyama vya siasa. Hata hivyo sheria hii haijawa wazi. Kifungu 6A (2) kinasema, "… Chama cha siasa kitasimamiwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Katiba ya Zanzibar, Sheria hii, katiba ya chama husika, kanuni za kidemokrasia, utawala bora, kuepuka ubaguzi, usawa wa kijinsia, na kujumuisha jamii". Kuhusu uteuzi wa mgombea, kifungu kidogo cha 5 kinaeleza, "chama cha siasa kitapigania… usawa wa kijinsia, vijana na ujumuishi wa makundi yote kwenye: (a) kutunga na kutekeleza sera zake; (b) kuteua wagombea kwa ajili ya chaguzi; na (c) uchaguzi wa viongozi wa chama (mwandishi ameongeza msisitizo).

Vifungu vilivyorejewa hapo juu vinavitaka vyama vya siasa kuzingatia suala la usawa wa kijinsia wakati wa kutunga na kutekeleza sera zao. Hata hivyo, sheria hizi hazivilazimishi vyama vya siasa kutekeleza hilo. Hakuna kifungu maalumu cha kuvilazimisha vyama vya siasa wala chombo chenye mamlaka ya kulazimisha vyama vya siasa kufanya hivyo. Tangu kupitishwa kwa Sheria hii mpya ya vyama vya siasa ya mwaka 2019, vyama hivi tayari vimeshaendesha chaguzi zake za ndani.

Hata hivyo, bado mfumo dume uko dhahiri kwenye vyama vyote vinne vilivyofanyiwa utafiti. Kuweka hili bayana, viongozi wote sita wa juu wa vyama vya CCM na CHADEMA ni wanaume wakati CUF na ACT-Wazalendo wana kiongozi mmoja mwanamke kwenye ngazi ya kitaifa[7]. Mbali na matakwa ya Sheria ya vyama vya viasa inayoeleza kuwa vyama vya siasa visivyoheshimu sheria za nchi vitafutwa, Msajili wa Vyama vya Siasa hajawahi kukifuta chama cha siasa ambacho hakizingatii suala la usawa wa kijinsia kwenye mchakato wake wa ndani. Wadau[8] wamekuwa wakipigania mabadiliko ya sheria hii ili suala la usawa wa kijinsia na ujumuishi lizingatiwe na vyama. Pamoja na mengine mengi, mabadiliko ya sheriayanatakiwa yaweze kuvilazimisha vyama vya siasa kuzingatia usawa wa kijinsia kwenye mchakato wa kuwapata wagombea na uchaguzi ndani ya vyama.

[7]Viongozi wa kitaifa ni kundi la viongozi sita ambao ni Wenyeviti, Makamu wenyeviti (Zanzibar na Tanzania bara), Makatibu wakuu, Manaibu Katibu wakuu (Zanzibar na Tanzania bara). Vyama vyote vinne vimekuwa na nafasi hizo za uongozi isipokuwa ACT Wazalendo ambao wao wana Kiongozi Mkuu wa Chama na Mwenyekiti wa Chama kwa wakati mmoja.

[8] Tazama mapendekezo yaliyomo kwenye uchambuzi wa Twaweza unaoitwa 'Analysis of the Political Parties (Amendment) Act, 2018 by Twaweza East Africa, Legal and Human Rights Centre (LHRC) , Tanganyika Law Society (TLS), Media Council of Tanzania (MCT), Waandishi wa Habari za Maendeleo Zanzibar (WAHAMAZA) and Centre for Strategic Litigation Submitted to The Parliamentary Committee on Legal and Constitutional Affairs on January 17, 2019.

Tatizo lingine la mfumo wa sheria limejitokeza katika taasisi zilizopewa mamlaka ya kusimamia michakato ya ndani ya vyama. Sheria ya vyama vya siasa inampa mamlaka Msajili wa Vyama vya Siasa kufuatilia chaguzi za ndani ya vyama vya siasa na michakato ya teuzi za wagombea. Hata hivyo, sheria hiyo haijaweka bayana kuhusu nini kinatakiwa kufuatiliwa kwenye vyama hivyo vya siasa, namna ya kufuatilia na kwa madhumuni gani. Lakini vilevile, Sheria haisemi ni kwa namna gani Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa itavilazimisha vyama vya siasa kuhakikisha usawa wa kijinsia unazingatiwa kwenye michakato yao ya ndani. Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa alithibitisha hilo wakati wa mahojiano kuwa ofisi ya Msajili wa vyama haina mamlaka mahususi yaliyowekwa kisheria ya kuvilazimisha vyama vya siasa kuzingatia suala la usawa wa kijinsia kwenye michakato ya ndani ya vyama, na matokeo yake, jukumu pekee la Msajili ni kuwa kama mshauri. Ofisi huandika barua kwenda kwenye vyama vya siasa kuwakumbusha kuzingatia kanuni za demokrasia kama vile usawa wa kijinsia[9]. Kwahiyo, jukumu la Msajili wa Vyama limebaki kuwa la uangalizi kinyume na lile la udhibiti.

Katika mahojiano mengine[10] ilionekana kuwa Ofisi ya Msajili wa Vyama haijawezeshwa kisheria kudhibiti mwenendo wa vyama vya siasa ili kuhakikisha kuwa suala la usawa wa kijinsia linazingatiwa. Katibu Mkuu wa CCM alieleza, “Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ni kama karani tu. Ofisi haina uwezo wa kufuatilia michakato ya ndani ya vyama. Endapo vyama vyote vya siasa vitaitisha mkutano mkuu ndani ya siku moja, je Msajili wa Vyama atakuwa na uwezo wa kuvifuatilia vyote?”[11] Kwa hakika, ni jambo lisilowezekana kabisa kwa Ofisi ya Msajili wa Vyama ambaye hana nguvu kazi ya kutosha, kuweza kufuatilia michakato ya ndani ya vyama vyote nchini. Msajili wa vyama hana mifumo na wafanyakazi waliosambaa nchi nzima ili ofisi iweze kufuatilia kila kinachoendelea ndani ya vyama vya siasa.

Miongoni mwa sababu zinazoifanya Ofisi ya Msajili wa Vyama kutokuwa na meno katika kuvilazimisha vyama vya siasa kuzingatia usawa wa kijinsia ni udhaifu uliomo katika muundo mzima wa sheria iliyounda ofisi hiyo. Kwa sasa, Rais – ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama kilichoko madarakani – humteua Msajili wa Vyama vya Siasa. Kwa utaratibu huo, inawezekana ikawa vigumu kwa Msajili wa Vyama kumlazimisha Rais na chama chake kuheshimu sheria za nchi. Kuna malalamiko mengi yaliyoenea sana kuwa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa siyo chombo huru, bali kinafanya kazi kwa maslahi ya chama tawala kuvikandamiza vyama vingine vya upinzani[12]. Kitendo cha kushindwa kuchukua hatua dhidi ya chama tawala inaonesha wazi kuwa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa haiwezi kuwa na nguvu ya kuviamrisha vyama vingine.

Kifungu pekee cha sheria ambacho kinasimamia uwepo wa wawakilishi wanawake ni kile cha sheria ya viti maalumu. Ibara ya 66 (1(b) na 78 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Kifungu cha 86A cha Sheria ya Uchaguzi ya 1985 vinaelekeza kuwa lazima kuwepo na asilimia 30 ya viti vya wabunge wanawake katika Bunge la Muungano. Vilevile, kifungu cha 35(1 (c) cha Sheria ya Serikali za Mitaa ya 1982 kinaelekeza kuwa lazima theluthi moja ya madiwani kwenye halmashauri husika wawe ni wanawake. Sheria kuhusu viti maalumu ililenga kuwa njia ya muda mfupi ya kukabiliana na tatizo la kihistoria la ubaguzi dhidi ya wanawake nchini. Ukweli ni kwamba, idadi kubwa ya wabunge wanawake imekuwa ikitokana na mfumo huu wa kuingia bungeni kwa mlango wa viti maalumu. Kati ya wabunge wanawake 138 wa bunge la 2015, wabunge 113 waliingia kwa njia ya viti maalumu, au sawa na asilimia 82 ya wabunge wote wanawake (NEC, 2016:68).

[9]Mahojiano na Bw. Sisty Nyahoza, Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa yaliyofanyika tarehe 12 Juni 2020.

[10] Tazama orodha iliyoambatanishwa kwenye Kiambatisho namba 1 chenye orodha ya watu waliohojiwa.

[11]Mahojiano na Dkt. Bashiru Kakurwa Ally, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) tarehe 6 Julai 2020.

[12]Mahojiano na maofisa mbalimbali wa vyama vya upinzani na Asasi za Kiraia.

Kuna mitazamo tofauti kuhusu mchango wa viti maalumu katika kupigania ushiriki na uwakilishi wa wanawake kwenye uongozi wa siasa. Kwa upande mmoja, ubunge wa viti maalumu unaonekana kuwa ni mkakati muhimu wa kuongeza idadi ya wanawake katika vyombo vya uwakilishi katika jamii iliyotawaliwa na mfumo dume kwa muda mrefu kama Tanzania. Kwa upande mwingine, mfumo wa viti maalumu unawalemaza wanawake wengi kiasi kwamba wanashindwa kuwa na ujasiri wa kwenda kupambana majimboni. Wale wanaounga mkono viti maalumu wanasema kuwa viti maalumu ni muhimu kwa sababu vinawajenga wanawake na hivyo baadaye kuwa na uwezo wa kugombea kwenye majimbo na kata. Kwa mfano, wanawake wengi waliochaguliwa kwenye majimbo mwaka 2015 waliwahi kuwa wabunge wa viti maalumu. Pamoja na kutambua mafanikio ya wanawake kugombea kupitia viti maalumu, wanaounga mkono uwepo wa viti hivyo wanapendekeza kufanyika kwa mabadiliko ya kisheria ili wanawake walioko kwenye viti maalumu wasikae zaidi ya mhula mmoja au miwili ili kuwawezesha wanawake wengi zaidi kugombea na kushika nafasi mbalimbali za kisiasa.[13]

Wakosoaji wa viti maalumu wanaeleza kuwa mbali na idadi ya wabunge wanawake kuongezeka bungeni, sheria hii haijatoa uhakika wa uwakilishi wa kudumu (Makulilo, 2009; Guariso na wenzake 2017; Edgell, 2018;). Kwa kulinganisha na mifano ya nchi nyingine kama Kenya na Uganda, Edgell anaonesha kuwa mara chache sana wanawake wamekuwa wakizidi asilimia ya viti maalimu iliyowekwa kisheria na hivyo swala hili linaweza kuwa na athari kubwa katika uwakilishi wa wanawake kwenye siasa. Anazidi kueleza kuwa, ili mfumo wa viti maalumu uweze kuleta matokeo ya muda mrefu ya uwakilishi wa wanawake, mfumo huyo inabidi utengenezwe kuendana na mazingira mengine yanayowaathiri wanawake mbali na mgawanyo wa viti maalumu.

Guariso na wenzake (2017) wanaeleza sababu tatu za kupinga mfumo wa viti maalumu. Sababu ya kwanza ni kuwa nchi nyingi za kiafrika kwa asili yake zina utawala wa kimabavu. Kwa mazingira hayo, uwepo wa mgawanyo wa madaraka kijinsia hakutasaidia mabadiliko ya sera (ili kuwa na uwakilishi mkubwa), labda itokee kuwa sera hii ya mgawanyo wa nafasi za madaraka kwa kuzingatia usawa wa kijinsia ianzie kwenye ngazi za juu za utawala na siyo kuwa ni suala la viti maalumu bungeni na kwenye baraza la wawakilishi bali lizingatiwe pia kwenye mihimili mingine ya dola – jambo ambalo kwa Tanzania bado haliwezekani. Mfano mmojawapo unaoonesha kuwa kuna ukosefu mkubwa wa dhamira ya kuleta usawa wa kijinsia ni uamuzi wa serikali kuwaachisha masomo wasichana wanaopata ujauzito wakiwa shuleni nchini Tanzania. Mwitikio wa wanawake wabunge waliopaza sauti zao kupinga maamuzi hayo ulikuwa chini sana. Moja ya sababu ya mwitikio huo mdogo ni pamoja na kuwa wanawake wa viti maalumu ambao ndio wengi bungeni wamekuwa watiifu zaidi kwa vyama vyao kuliko maslahi mapana ya wanawake wenzao (Lohmann, 2019).

[13]Mahojiano mbalimbali

Sababu ya pili ni kuwa bado mfumo dume unatawala kwenye jamii, vyama na makabila, yote hayo yanafunika kabisa suala la kuwa na usawa wa kijinsia kwenye siasa. Jamii iliyogawanyika kwa misingi ya ukabila, masuala ya haya yanachukua nafasi ya kubwa zaidi kuliko usawa wa kijinsia. Utaona kuwa usawa wa kijinsia linakuwa ni suala lisilo na umuhimu kabisa kwenye jamii kama hizo. Kwahiyo, suala la usawa wa jinsia na ushiriki wa wanawake katika siasa ndani ya vyama vikuu haliwezi kuchukuliwa kama suala la msingi sana katika jamii ya Tanzania.

Sababu ya tatu ni kuwa nadharia ya mrengo wa haki za binadamu ya kupigania haki na uwezeshaji wa wanawake unaweza usifanikiwe kuleta mabadiliko ya mifumo ya kijamii kwakuwa wanawake wamekuzwa katika mifumo hiyo ya kijamii iliyomfanya yeye aonekane kiumbe dhaifu na mnyonge toka zamani. Hivyo, hata kama kutakuwa na mabadiliko kwenye mifumo rasmi ya uwakilishi, bado kunaweza kusitokee mabadiliko makubwa kwa wanawake kwani wanaweza wakaendelea kudumu katika hali hiyo kutokana na mifumo hiyo ya kijamii. Hali hii inaweza kueleza kwanini uwakilishi wa wanawake katika ngazi za majimbo ya uchaguzi Tanzania ni mdogo. Hii ni kwasababu michakato ya teuzi za wagombea ndani ya vyama inafanya wanawake kujielekeza zaidi kwenye nafasi za viti maalumu na hivyo kuacha nafasi za kugombea katika majimbo zinachukuliwa na wanaume[14]. Wadau[15] mbalimbali walieleza kuwa viti maalumu vinawanyima wanawake wengi nafasi ya kugombea kwasababu wanajiona wao ni wa viti maalumu[16] tu na si vinginevyo. Hivyo, viti maalumu ni njia ya wanawake kuingia kwenye nafasi ya uwakilishi bila ya kuathiri mfumo dume uliopo katika nafasi za kuchaguliwa nchini Tanzania.

[14]Kama ilivyojitokeza katika mahojiano mengi

[15]Mahojiano na John Mnyika , Katibu Mkuu wa CHADEMA); Zitto Zuberi Kabwe, Kiongozi Mkuu wa Chama, ACT-Wazalendo; Savelina Silvanus Mwijage aliyewahi kuwa Mbunge Viti Maalumu (CUF) na Mjumbe wa Halamshauri Kuu ya Taifa (NEC) ACTWazalendo; Anatropia Theonest aliyekuwa mgombea wa Jimbo la Segerea na Mbunge wa Viti Maalumu, CHADEMA.

[16]Mahojiano na wadau mbalimbali

# Sheria na kanuni za vyama na uwakilishi wa wanawake

Sehemu hii inaangazia jinsi kanuni za vyama zinavyoathiri usawa wa kijinsia na uwakilishi wa wanawake wakati wa kuteua wagombea. Kwanza sehemu hii inalenga kuonyesha kama vyama vya siasa vinazingatia sheria za nchi na misingi ya demokrasia kama vile kutobagua wanachama, usawa wa kijinsia na mfumo jumuishi wakati wa kuandaa kanuni na kuzitekeleza. Pili, sehemu hii inaangazia jinsi vyama hivi vinne vilivyofanyiwa uchambuzi vinavyohimiza au kukwamisha upatikanaji wa wagombea wanawake. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa vyama vinazingatia sheria ya nchi, yaani katiba, katika kuandaa katiba zao, sera na kanuni. Kwa hakika vyama vimekuwa vikieleza kwenye katiba zao kuwa vitakuwa mstari wa mbele kusimamia kanuni za demokrasia, kutobagua na usawa wa kijinsia kwenye katiba, sheria na kanuni zao.[17]

Lakini linapokuja suala la utekelezaji, hakuna chama cha siasa kinachozingatia sheria za nchi wala kufuata kanuni zao wenyewe kuhusu usawa wa jinsia katika michakato yao ya ndani. Kama ilivyoonyeshwa mahali pengine katika chapisho hili, vyama vya siasa havizingatii usawa wa jinsia katika kuwapata wagombea na viongozi ndani ya vyama. Vinapendekeza na kuchagua zaidi wanaume kuliko wanawake. Zaidi ya hayo, vyama vya siasa havielezi namna gani vitazingatia kanuni za kidemokrasia zinazohusu usawa wa kijinsia, ushiriki, kutobagua, na utu kwa wote.

Katibu Mkuu wa CCM na Mkurugenzi wa Uchaguzi wa CHADEMA[18] walithibitisha kuwa tatizo kubwa la ndani ya vyama ni kusimamia kanuni za chama pamoja na misingi ya demokrasia. Walikiri kuwa hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya kinachoelezwa kwenye katiba na uhalisia wa kinachotendeka. Dkt. Bashiru Ally (CCM) anasema, kuna udhaifu mkubwa wa kimfumo na kiitikadi katikavyama, na ikitokea itikadi ikawa dhaifu, na mifumo ya kusimamia usawa wa kijinsia nayo inakuwa dhaifu".[19]

Zaidi, imebainika kuwa viongozi wengi wa vyama vya siasa wanatambua kuwa ingawa vyama vina kanuni na misingi ya demokrasia inayotambua usawa wa kijinsia, wanashindwa kutekeleza kanuni hizo ndani ya vyama vyao kwasababu ya imani iliyojikita katika mizizi ya mfumo dume kuwa wanawake hawachaguliki[20]. Kukabiliana na fikra kama hizi, vyama vya siasa vinawajengea uwezo wanawake ili waweze kuomba nafasi mbalimbali za uongozi na kugombea nafasi za uwakilishi. Uamuzi wa kuwajengea uwezo ni muhimu na ni mkakati mzuri, hata hivyo hautaleta mabadiliko yanayohitajika endapo mifumo na taratibu za kuwapata wagombea hazijawekwa kuhakikisha kuwa kuna usawa wa kijinsia. Makala hii imebaini kuwa mifumo ya upatikanaji wa wagombea ndani vyama imetawaliwa na mfumo dume. Ni mifumo iliyoandaa kanuni ambazo si rafiki kwa wanawake kugombea kwani wanatakiwa kuwa wenye uwezo wa kifedha, uzoefu katika uongozi na wawe na uwezo kupambana na kushinda chaguzi pindi wanapoteuliwa.[21]

---

[17]Ibara ya 4 (1) (2) ya Katiba ya CCM ya mwaka 1977 [iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2017]; Ibara ya 4.3.1ya Katiba ya CHADEMA, 2006 [kama ivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019]; Ibara ya 4 (2) (i) (ii); Ibara ya 6 (4) ya Katiba ya ACT-Wazalendo ya 2015; Ibara ya 6 (1(a-c) ya CUF toleo la 2014.

[18]Mahojiano na Dkt Bashiru Ally Kakurwa, Katibu Mkuu wa CCM na Gerald Munisi, Mkurugenzi wa Uchaguzi na Uratibu, CHADEMA

[19]Mahojiano na Dkt Bashiru Ally Kakurwa, Katibu Mkuu wa CCM

[20]Mahojiano na maofisa wa vyama

[21] Uwezo wa kushinda unapimwa na mambo mengi na miongoni mwa mambo hayo ni kukubalika mbele ya viongozi wa vyama, mamlaka za uteuzi, wajumbe na wapiga kura. Hii inamaanisha pia kuwa mgombea lazima awe na uwezo ya mali na uwezo wa kifedha, ingawa hili huwa haliko bayana sana kama matakwa ya kuteuliwa ndani ya vyama hivi vinne.

## UCHAMBUZI WA MUUNDO WA VYAMA VYA SIASA NA UWAKILISHI WA WANAWAKE

Vyama vinne vilivyofanyiwa uchambuzi vina mifumo ya kitaasisi inayofanana kwa sehemu kubwa kwani mifumo yao inaanzia ngazi ya taifa, mkoa, wilaya hadi kwenye mashina. Uchambuzi unaonesha kuwa vinatawaliwa kutoka makao makuu. Ngazi au vyombo vya maamuzi viko mikononi mwa Kamati Kuu, Halmashauri Kuu[22] (kwa upande wa CCM) na ACT-Wazalendo), Baraza Kuu la Uongozi kwa CHADEMA, Baraza la Viongozi wa Kitaifa kwa upande wa CUF, na vyama vyote hivi vina Mkutano Mkuu wa Taifa. Ukiachilia mbali wagombea wa udiwani, vyombo hivi vikuu vya kitaifa huamua nani agombee uraisi na ubunge.

Kama Schattschneider alivyoeleza hapo awali, uteuzi wa wagombea ni miongoni mwa mambo muhimu katika kuonesha mgawanyo wa madaraka ndani ya chama. Uchambuzi unaonesha kuwa kuna muunganiko mkubwa kati ya mamlaka ya kuteua na vyombo vya maamuzi ya ndani ya chama. Kwa mfano, wajumbe wote wa Kamati Kuu ya vyama ni wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa, wajumbe wa Baraza Kuu la Uongozi, wajumbe wa Baraza la Uongozi wa Taifa, huku mkutano mkuu ukiwa na wajumbe kutoka Kamati Kuu, Halmashauri Kuu/Baraza Kuu/Baraza la Uongozi. Mkusanyiko huu wa wajumbe kutoka vyombo vya maamuzi kwa sehemu kubwa umetawaliwa na wanaume. Ingawa data kuhusu wanawake kwenye nafasi za uongozi ndani ya vyama kuanzia ngazi ya chini hadi taifa hazikuweza kupatikana, viongozi wa kitaifa na kwenye vyombo vya maamuzi walio wengi ni wanaume. Kama ilivyoelezwa hapo awali, viongozi wote wa juu wa kitaifa wa CHADEMA na CCM ni wanaume, huku CUF na ACT-Wazalendo vikiwa na mwanamke mmoja kwenye ngazi ya kitaifa.

Mifumo dume imejidhihirisha pia kwenye vyombo vya maamuzi ngazi ya taifa. Kwa upande wa CCM kati ya wajumbe[24] wa Kamati Kuu, wanawake ni wanne tu[23]. Katiba ya CHADEMA ya mwaka 201924 inaeleza kuwa wanawake wanapewa nafasi saba kati ya wajumbe 60 wanaounda Kamati Kuu. Wakati wa mahojiano na ofisa kutoka CHADEMA, ilidhihirika kuwa kwa sasa wajumbe wa Kamati Kuu wako 42, na kati yao wanawake ni 9 tu[25]. Katiba ya CUF ya mwaka 2014 inaeleza kuhusu idadi ya wajumbe wanaoshiriki mkutano wa Baraza Uongozi Taifa kuwa ni 68, na kati ya hao nafasi 19 zimetengwa maalumu kwa ajili ya wanawake[26]. Katiba ya Chama cha ACT-Wazalendo ya mwaka 2015 inaeleza kuwa wajumbe wa Kamati Kuu watakuwa 54 na wana nafasi 5 tu za wajumbe wanawake kikatiba. Nafasi hizo tano ni za mwenyekiti na katibu wa umoja wa wanawake na wengine watatu watateuliwa na kiongozi wa chama[27]. Mikutano Mikuu kwa vyama vyote vinne vina wajumbe wanaume wengi zaidi kuliko wanawake[28].

Kama ilivyo kwa vyombo vikuu vya maamuzi, wajumbe wa mkutano mkuu ni wale wanaofika kwa mgongo wa vyeo vyao. Na nafasi nyingi za uongozi kwenye vyama zinashikiliwa na wanaume. Huku jinsia ya wajumbe wengine wachache wanaobaki ikitegemea nafasi zao kwa mujibu wa katiba za vyama. Jitihada za kupata idadi halisi kulingana na jinsia kuanzia ngazi ya kitaifa, kimkoa na kiwilaya zilifanyika wakati wa mahojiano na

[22] CHADEMA waita Baraza Kuu na CUF wanaita Baraza la Uongozi Taifa.

[23]Baraza la Kitaifa la Uongozi la CUF

[24]Tazama Ibara ya 103 (1(a-s) ya Katiba ya CCM ya 2017 kwa ajili ya orodha ya wajumbe wa Kamati Kuu. Kumbuka kuwa Katiba haielezi kuhusu muundo wa Kamati kwa kuzingatia jinsia wala haifafanui kuhusu idadi inayotakiwa kwa mgawanyo wa jinsia. Kama nafasi zote za uongozi zitashikiliwa na wanaume basi kuna uwezekano mkubwa wa Kamati Kuu zote kuwa na wanaume watupu.

[25]Soma Ibara ya 7.7.14 ikisomwa pamoja na Ibara ya 7.7.17 kwa ajili ya kuelewa kuhusu orodha ya wajumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA.

[26]Mahojiano na Elizabeth Donatus Massanja, Mratibu wa Taifa, Baraza la Wanawake CHADEMA (BAWACHA), 13 Juni 2020.

[27]Baraza Kuu la Uongozi Taifa. Soma Ibara ya 81(1(i-xii) ya Katiba ya CUF toleo la 2014

[28]Soma Ibara ya 12 (i-xiv) ya Katiba ya ACT-Wazalendo, 2015

viongozi wa juu wa vyama. Hata hivyo haikuwa rahisi kupata data hizo. Baadhi ya maofisa wa vyama walitoa taarifa zinazokinzana. Ili kuepuka kuwa na taarifa za kubuni, mtafiti aliona bora ajikite zaidi kwenye vipengele vya katiba za vyama. Pia, jitihada za kupata data za uongozi ndani ya vyama zilifanyika kwa kuwasiliana na Ofisi ya Msajili wa Vyama, bahati mbaya ofisi hiyo ina taarifa za viongozi wa kitaifa pekee[29].

Kitendo cha maamuzi yote kufanywa makao makuu ya vyama, yakiwemo yanayohusu kuteua wagombea, kinaonesha kuwa hakuna demokrasia ndani ya vyama na hivyo kurudisha nyuma jitihada za wanawake kuingia kwenye nafasi za uongozi. Zaidi ya hayo, kitendo cha wanaume kutawala mifumo yote na kutunga kanuni ambazo zinawanufaisha wao wenyewe kinafanya mchakato wa kumkomboa mwanamke kuwa mgumu hasa kwenye uteuzi wa wagombea (IDEA, 2005). Sehemu ndogo zinazofuata zinaangazia sifa za kuteuliwa na taratibu zake ili kuonesha wazi namna gani zinakwamisha ushiriki wa wanawake kwenye siasa.

## SIFA ZA KUGOMBEA

Vyama vyote vinne vinaelezea sifa za kuwa mgombea kupitia vyama hivyo. Miongoni mwa sifa hizo ni pamoja na: uanachama, kukubalika na wanachama na wapigakura, uadilifu, uzoefu katika uongozi, kukidhi matakwa ya katiba ya nchi, uelewa kuhusu itikadi ya chama, kuwa mkweli, mchapakazi, na kiwango cha elimu[30]. Ingawa wanaume na wanawake wanaweza kwa pamoja kuwa na sifa hizo zote, bado utaona wanawake wanatakiwa kuonesha uwezo wao zaidi kama wana sifa za kushinda, wanatakiwa wajulikane kwa viongozi wa chama, wanachama na wapiga kura ili waweze kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za kisiasa[31]. Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Bw. Zitto Zuberi Kabwe, anasema kuwa masharti hayo ya nyongeza yanatokana na mitazamo iliyopitwa na wakati ndani ya vyama na uongozi wa vyama kuwa wanawake hawachaguliki[32].

Mbali na sifa za kuteuliwa za hapo juu, wanachama wanatakiwa kutoa kiasi cha fedha kwa ajili ya kuchukua fomu za kuomba uteuzi. Kiwango cha fedha hizi kinatofautiana kutegemea na nafasi ambayo mgombea anaiomba lakini pia kila chama cha siasa kina kiwango chake. Kwa mfano wanachama wa CCM wamekuwa wakitoa kati ya shilingi 10,000 kwa madiwani, 100,000 kwa wabunge na milioni moja kwa wagombea wa urais[33]. Kwa upande wa CHADEMA na ACT-Wazalendo wagombea wa urais walitoa shilingi milioni moja, huku wagombea wa ubunge walichangia laki moja na udiwani elfu ishirini[34]. Chama cha Wananchi (CUF) kilitoza elfu kumi kwa wagombea wa udiwani, 50,000[35] kwa wabunge (wa majimbo na wa viti maalumu) na laki tano kwa wagombea wa urais. Mbali na kiwango kinachotolewa kwenye vyama, sheria ya uchaguzi ya Tanzania inawataka wagombea kulipia ada ya uteuzi kwa Tume ya Uchaguzi[36].

[29]Vyama vina vifungu mahususi kwenye Katiba zao vinavyozungumzia usawa wa kijinsia kwenye nafasi za uteuzi za wenyeviti wa vyama na wajumbe wa Kamati Kuu, Halmashauri Kuu na mkutano mkuu. Soma vifungu hivyo kwenye vyama: soma Ibara ya 7.7.11 (g) & 7.7.14 (q) ya Katiba ya CHADEMA ya 2006 [iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019]; soma Ibara ya 108 (o) Katiba yof CCM; soma Ibara ya 78 (1) (l) (m) (n) (o) na Ibara ya 81 (1) (viii) (ix) (x) ya Katiba ya CUF ya mwaka 1992 [kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2014]; soma Ibara ya 29 (4) (iv) (v), (8) (ix), (12) (x) ya Katiba ya ACT-Wazalendo ya mwaka 2015.

[30]Soma Kanuni za Uchaguzi za CCM za mwaka 2019 kifungu cha 57; Ibara ya 10(1(iii) ya Katiba ya ACTWazalendo ya mwaka 2015; Katiba ya CUF 2014 ; Kanuni za Uchaguzi za CUF za mwaka, 2013 ; Kifungu cha 7.5 cha Katiba ya CHADEMA ya mwaka 2016.

[31]Mahojiano na Zitto Zuberi Kabwe, Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, 14 Julai 2020.

[32]Mahojiano na maofisa wa vyama, wabunge wa zamani wanawake, na wagombea

[33]Kifungu cha 11 (1) cha Kanuni za Uteuzi wa Wagombea Uongozi Katika Vyombo vya Dola (toleo la 2019).

[34]Mahojiano na maofisa wa vyama cha CHADEMA na ACT- Wazalendo

[35]Wanawake wanaotaka kugombea ubunge kupitia Viti Maalumu watatakiwa kulipia fomu kwa shilingi za Kitanzania 100,000.

[36]Kifungu namba 33 (1) cha Sheria ya Uchaguzi (Iliyoboreshwa) Na. 2 ya mwaka 1992

Tafiti za huko nyuma zimeonesha kuwa fedha hizi zinazotolewa kwenye vyama kwa ajili ya kuomba kuteuliwa zimekuwa zikiwafanya wanawake wengi kushindwa kugombea nafasi mbalimbali za uongozi (Shayo, 2005; Makulilo, 2014; Meena & Makulilo 2015). Wakati wa mahojiano na viongozi wa vyama vya siasa, hasa wale wa kutoka jumuiya za wanawake wa vyama hivi vinne pamoja na wanaharakati na asasi za kiraia, imebainika kuwa fedha hizi za kulipa kwenye vyama kwa ajili ya kuomba uteuzi zimekuwa kikwazo kwa wanawake wengi wanaopenda kugombea[37]. Lakini changamoto kubwa zaidi kwa wanawake ni kuhusu gharama za kufanya kampeni[38]. Rasilimali nyingi zinahitajika kufanya kampeni wakati wa mchakato wa ndani ya vyama na wakati wa kushindana majukwaani na wagombea wa kutoka vyama vingine. Ukosefu wa fedha ni kikwazo kikubwa kwa wanawake wengi kushindwa kuingia katika madaraka[39]. Utafiti wa IDEA unasisitiza kuwa "gharama za kufanya kampeni zinasababisha kukosekana kwa fursa sawa kwa makundi yote kushindana kwa haki kwenye siasa. Wale wenye fedha za kutosha, wenye mitandao ya kupata fedha, viongozi na wakongwe wa siasa wanakuwa na nafasi kubwa zaidi ya kufanya vizuri kwenye siasa kuliko wengine. Hili liko bayana sana unapoangalia athari za ukosefu wa fedha kwenye siasa kwa wagombea wanawake katika uchaguzi"(2014:301).

Ukosefu wa fedha unawaathiri wanawake kwasababu wao mara zote wanakabiliwa zaidi na changamoto za kiuchumi na pia kijamii wanatengwa, na wengine wanaishi katika umaskini mkubwa, hawana elimu ya kutosha na hata wale walio kwenye ajira hupata ujira mdogo au kutolipwa ipasavyo. Mathalani, Illesanmi (2018) anaeleza kuwa wanawake wa kiafrika hutengwa sana katika kufanya maamuzi na ndio kundi lililobaki katika umaskini mkubwa ukilinganisha na wenzao wanaume. Hoja hii inasisitizwa zaidi na Odhiambo (akinukuliwa na Anyango, Alupo, & Opoku, 2018) akieleza kuwa umaskini ndani ya kaya na maeneo ya vijijini umewaathiri zaidi wanawake na hivyo ipo haja kubwa ya kuwawezesha kiuchumi.

Ukosefu wa fedha umewafanya wanawake wengi kushindwa kulipia fomu za kuomba uteuzi ndani ya vyama na kulipia ada za kisheria zinazohusu uchaguzi Tanzania. Kwa baadhi ya kaya, wanawake hawawezi kugombea mpaka wapewe ridhaa na waume zao na hii imekuwa pia kikwazo kikubwa cha wanawake kushindwa siyo tu kilipia fomu bali pia kutoweza kushiriki katika shughuli za kisiasa na uchaguzi. Kama ambavyo Lohmann (2019: 7) ananukuliwa, "katika jamii nyingi za kiafrika ambako mume anakuwa na sauti juu ya matumizi ya kwenye kaya, wanawake ambao wangependa kushiriki kwenye siasa lazima waombe ruhusa kwa waume zao siyo kwa ajili ya kushiriki kwenye siasa bali pia kuomba kibali cha kutumia fedha ya familia".

## KUCHUJA, KUPIGA KURA NA MAAMUZI YA MWISHO

Eneo lingine linalokwamisha ushiriki wa wanawake katika kugombea linahusu mchakato wa kupitia majina ya wagombea. Baada ya wanachama kuonesha nia za kugombea, huchukua fomu na kuzirejesha na kulipia fedha za kuchukulia fomu. Baada ya zoezi hilo, vyama vya siasa huendelea na mchakato wa kupitia majina ya wagombea na baadaye kufanya uteuzi na kutangaza wagombea.

Jukumu la kuwachuja wagombea wa urais na kuwatangaza liko kwenye vyombo vya maamuzi ngazi ya taifa, na hili lipo kwa vyama vyote. Kuhodhiwa kwa madaraka hayo ya uteuzi na mamlaka za juu za vyama kumejitokeza kwa vyama vyote vinne. Kutokana na ukweli kuwa walioko kwenye Kamati Kuu za vyama ndio hao hao wako pia kwenye ngazi nyingine za maamuzi, inakuwa vigumu kwa ngazi nyingine za vyama kupinga maamuzi ya Kamati Kuu na badala yake kuwa na jukumu la kupitisha kwa sauti moja kile

[37]Mahojiano mbalimbali na viongozi wa wanawake wa vyama na asasi za kiraia.

[38]Mahojiano na viongozi wa vyama, matawi ya wanawake, viongozi wa asasi za kiraia na wanaharakati kama inavyooneshwa kwenye Kiambatisho Na 1.

[39]Kama ilivyojitokeza kwenye mahojiano yote yaliyofanyika.

kilichoamriwa na Kamati Kuu. Hali iko hivyo kwa vyama hivi vinne ambapo ofisi zao za mkoa zimepewa mamlaka ya kuamua kuhusu wagombea wa udiwani kwenye kata za mkoa husika. Hata hivyo, kuna tofauti kidogo kati ya vyama hivi vinne kuhusu uteuzi wa wagombea wa ubunge.

Kwa upande wa CCM, wagombea wote wa nafasi za ubunge wanajadiliwa na kamati za siasa za majimbo, wilaya na mkoa. Kamati hizi zinapeleka mapendekezo yao kwenye Kamati Kuu. Hatua zinazofuata ni kwa Kamati Kuu kutathmini mapendekezo hayo na kuchagua majina yasiyozidi matatu yatakoyorudishwa kwenye mkutano mkuu wa jimbo (kwa upande wa Zanzibar) na mkutano mkuu wa wilaya (kwa upande wa Tanzania bara)40. Wagombea hao watatu watapigiwa kura na baadaye ripoti ya upigaji kura inarejeshwa tena Kamati Kuu kwa kufanyiwa tathmini na baadaye kupelekwa kwenye Halmashauri Kuu kwa ajili ya uteuzi. Kwa namna yoyote ile, inatarajiwa kuwa Halmashauri Kuu itawateua wagombea waliopata kura nyingi zaidi ya wengine[41]. Hata hivyo, hali imekuwa tofauti kwani Halmashauri Kuu haiteui wagombea kwa kuzingatia uwingi wa kura ambazo mgombea amepata[42]. Mchakato wa hivi karibuni wa kuwapata wagombea ndani ya CCM kwa mwaka 2020 umeonesha kuwa Halmashauri Kuu ndio yenye maamuzi ya mwisho kuhusu nani anagombea na nani hagombei na siyo kwa kuzingatia idadi ya kura ambazo mtu amepata. Utaratibu uliotumika mwaka 2020 umekuwa tofauti na ule uliotumika miaka ya nyuma. Wagombea walichukua fomu na kupigiwa kura na mkutano mkuu wa wilaya na wa jimbo kabla ya kupitishwa na kutangazwa na vyombo vya maamuzi vya ngazi ya kitaifa.

Mtindo wa kuteua wagombea unaofanywa na vyombo vya mamlaka ngazi ya taifa tulioona kwa CCM unatumika pia na vyama vingine vitatu huku kukiwa na tofauti ndogo za kiutendaji. Ingawa, viongozi wa kitaifa wanafanya maamuzi kuhusu wagombea kwa kuzingatia tathmini, uchambuzi, na kura walizopata kutoka ngazi za chini (wilayani na mkoani). Kwa upande wa wabunge/ wawakilishi ndani ya CUF, uchambuzi unafanywa katika ngazi ya jimbo au wilaya na baadaye kwenye Kamati Kuu ya chama. Uamuzi wa mwisho unafanywa na Baraza Kuu la Uongozi wa Kitaifa[43], sawa na inavyofanyika kwa Halmashauri Kuu ya CCM, lakini wenyewe wanakuwa na wajumbe wachache zaidi. Tofauti na vyama vingine, Katiba ya CUF iko bayana kabisa kuhusu mgawanyo wa kijinsia kwenye muundo wake wa Baraza Kuu la Viongozi wa Taifa. Katiba ya CUF inaeleza bayana kuwa kati ya wajumbe 69 wa baraza hilo la viongozi lazima wajumbe wanawake wawe 19, ambao ni sawa na asilimia 28 ya wajumbe wote. Afisa Uratibu na Uongozi wa CUF alithibitisha hilo wakati wa mahojiano kuwa kwa sasa Baraza kuu la Viongozi wa Taifa lina wajumbe 75 na wanawake ni asilimia 30 ya wajumbe wote[44].

Utaratibu huo upo pia ndani ya CHADEMA na ACT-Wazalendo ingawa kwa upande wao ni Kamati Kuu ndiyo inayofanya maamuzi ya mwisho kuhusu wagombea wa ubunge. Baada ya vyombo vya maamuzi ngazi ya jimbo, wilaya na mkoa kufanya uchambuzi wa wagombea, majina ya wagombea na kura walizopata hupelekwa makao makuu ya chama ambako Kamati Kuu hukaa kuyapitia na kufanya maamuzi ya kuwateua wagombea45.

[40]Kifungu cha 12 (iv) cha Kanuni za Uteuzi wa Wagombea Uongozi Katika Vyombo vya Dola (toleo la 2019).

[41]Kifungu cha 16 (1) cha Kanuni mpya za uchaguzi za CCM za mwaka 2019 zinawataka wagombea kupata kura za kutosha (zaidi ya asilimia 50 ili watangazwe washindi. Huko nyuma, kanuni ilikuwa yeyote anayepata kura za kumzidi mshindani wake anakuwa mshindi. Itapendeza zaidi kufuatilia utekelezaji wa kanuni hii na itakavyomaanisha kwa wanawake kwenye uchaguzi wa 2020 na kama kanuni hii itatumika.

[42]Kifungu cha 16(1) cha Kanuni za Uteuzi wa Wagombea Uongozi Katika Vyombo vya Dola (toleo la 2019)

[43]Baraza Kuu la Uongozi, CUF

[44]Kwa ajili ya muundo wa wajumbe wa Baraza la Uongozi Taifa la CUF soma Ibara ya 81(1(i-xiii) ya Katiba ya CUF ya mwaka 2014.

[45]Ibara ya 7.7.16 (q) ya Katiba ya CHADEMA ya mwaka 2019 na Ibara ya 29 (13) (xvii) ya Katiba ya ACT-Wazalendo ya mwaka 2015.

Wakati CHADEMA ina wajumbe 60 wa Kamati Kuu, kwa upande wa ACT-Wazalendo wako 5446. Kama inayoonekana, kamati hizi zenye maamuzi ya mwisho ndani ya hivi vyama siyo tu zimeundwa na watu wachache bali pia kuna uwezekano mkubwa kusiwepo na uwiano wa kijinsia. Hii inatokana na ukweli kuwa wajumbe wanateuliwa na viongozi/maofisa wa chama ngazi ya taifa, ambao wengi wao ni wanaume.

Taratibu za kuwateua wagombea kama ilivyoelezwa hapo juu zina athari tatu kwa wanawake. Kwanza, mchakato unatawaliwa na maamuzi ya viongozi wa juu wa kitaifa ambao ndio wenye mamlaka makubwa ya kuamua nani awe mgombea na nani asipitishwe kuwa mgombea. Pili, uteuzi wa wanawake kama wagombea utategemea zaidi utashi wa kisiasa wa vyombo vya maamuzi vya kitaifa, yaani Kamati Kuu, Halmashauri Kuu, Baraza la Uongozi na Baraza la Viongozi wa Taifa. Upigaji kura unaofanywa na ngazi za chini siyo unaoamua moja kwa moja nani awe mgombea na uamuzi wa ngazi za chini unaweza usitumike kama mwongozo wa maamuzi kwa viongozi wa ngazi ya kitaifa[47]. Uzoefu unaonesha kuwa vyombo vya maamuzi vya ngazi ya taifa vimekuwa vikiweka majina ya wagombea wengine kinyume na maamuzi ya mikutano mikuu ya wanachama ngazi ya jimbo au wilaya. Mathalani, mwaka 2010 CCM iliteua wagombea tofauti kabisa na wale waliochaguliwa na wanachama ngazi za majimbo[48]. Hata hivyo baadhi ya mabadiliko hayo yalilenga kuwapendelea wagombea wanawake kwa baadhi ya majimbo kama vile Iringa Mjini na Handeni Vijijini. CHADEMA ilimuengua mgombea mwanamke na kuteua mwanaume katika jimbo la Moshi Vijijini. Tatu, utaratibu wa uteuzi wa wagombea kwenye vyama hivi umekuwa ukibadilishwa mara kwa mara. Kwa mfano, CCM kwa mwaka 2020 imeruhusu wajumbe wa mkutano mkuu wa jimbo/wilaya kuwapigia kura wagombea kabla ya kuwachuja na kupitisha majina ya mwisho ya wagombea. Bado haijulikani kama wanawake watapata nafuu kupitia utaratibu huu mpya ama la49. Kwahiyo, ni muhimu kuangalia michakato ya uchaguzi na kuchambua masuala yanayojitokeza kuhusiana na usawa wa kijinsia kabla ya mchakato wa kuwapata wagombea na baada ya mchakato wa uchaguzi wa 2020 kukamilika. Vivyo hivyo, itakuwa jambo la muhimu kufuatilia na kuweka msisitizo kuhusu namna vyama vya siasa vinazingatia kanuni zao au kupindisha kanuni zao wenyewe na hayo yanayofanyika yana athari gani kwa wanawake. Ni muhimu pia kwa vyama vya siasa kuandaa taratibu za kusimamia teuzi za wagombea na kuweka mifumo ambayo itasimamia usawa wa kijinsia ndani ya vyama wakati wa kuteua wagombea.

---

[46]Takwimu hii, kama ilivyoelezwa hapo awali, siyo za uhakika sana. Zimetokana na hesabu za mwandishi kulingana na vifungu vya katiba za vyama kuhusiana na vyombo vya ngazi za juu za maamuzi.
[47]Kanuni za Uchaguzi za CCM za mwaka 2019 zinaeleza kuwa utaratibu wa kupiga kura ngazi ya majimbo na wilaya haumaanishi kuwa ndio unaoamua mshindi bali ni kiashiria tu cha kiwango cha kuungwa mkono kwa mgombea na ngazi za chini za chama (soma Kanuni za CCM za 2019, uk. 35).
[48]Soma MwanaHalisi, tarehe 18 Agosti, 2010; Mwananchi, 20 Septemba, 2010; TEMCO, 2011; TEMCO, 2016.
[49]Ikumbukwe kuwa huko nyuma, wagombea wote walipigiwa kura na mkutano mkuu wa jimbo au wilaya kabla ya kuchunguzwa na kupitishwa na vikao vya ngazi za juu. Ni majina matatu tu ya wagombea waliopata kura nyingi ndio yaliyokuwa yanapelekwa kwenye vikao vya juu vya chama kwa ajili ya maamuzi. Kama ilivyoelezwa hapo awali, ni vizuri kusubiri kuona mabadiliko haya ndani ya CCM yatakavyokuwa na athari kwa wanawake. Ikumbukwe kuwa kanuni hizi huweza kubadilishwa wakati wowote na ngazi za juu.

# Hitimisho na mapendekezo

Utafiti huu ulilenga zaidi kuangalia namna vyama vinavyoendesha michakato ya ndani ya kuwapata wagombea, mifumo ya kisheria na mifumo ya taasisi zinazosimamia michakato hiyo, na namna mambo hayo yanavyoathiri ustawi wa demokrasia na uwakilishi wa wanawake nchini Tanzania. Kwa ujumla, uchambuzi huu unaonesha kuwa kuna udhaifu mkubwa katika sheria za nchi na mifumo ya kitaasisi katika kuvilazimisha vyama vya siasa kuzingatia usawa wa kijinsia kwenye michakato yao ya kupata wagombea. Kwa hakika, Ofisi ya Msajili wa Vyama ni kama mbwa asiye na meno kutokana na udhaifu mkubwa wa kimuundo na rasilimali katika kuvisimamia vyama vya siasa. Pia, mapitio ya katiba za vyama yanaonesha kuwa vyama vya siasa vinatambua utu wa mwanadamu, usawa wa kijinsia, haki, demokrasia, uwazi na uwajibikaji. Lakini hayo yamo kwenye makaratasi tu na siyo kwenye utendaji.

Sheria za vyama zinasisitiza kuhusu umuhimu wa kuwa na siasa jumuishi na zisizo na ubaguzi katika misingi ya jinsi, rangi, kabila, dini, itikadi, utamaduni, hali ya kiuchumi na maumbile. Hata hivyo, vyama vingi havijaweza kuzingatia usawa wa kijinsia kwa vitendo katika michakato yake ya ndani. Mathalani, hakuna chama kilichoweza kusimamia vya kutosha masuala ya usawa wa kijinsia wakati wa mchakato wa kuwapata na kuwateua wagombea mbali na kuwa kwenye katiba zao wanaeleza kuwa wanaamini katika usawa wa kijinsia. Zaidi ya hayo, inaonesha kuwa vyama vyote vinne havina uwazi katika kuendesha mchakato wa kupata wagombea kwani mchakato umehodhiwa na viongozi wa kitaifa50 na umekuwa ni utaratibu uliozoeleka na waj kawaida kwenye hivi vyama.

Mbali na udhaifu huo ulioelezwa hapo juu kwenye mifumo ya kisheria ya vyama hivi, utafiti huu umebaini pia vikwazo vingine vinavyowafanya wanawake wasijitokeze katika ulingo wa kisiasa kama wagombea na viongozi. Matatizo haya yameota mizizi kwenye mfumo dume unaowabagua wanawake, mazingira ya kisiasa yasiyo rafiki kwa wanawake, viwango vidogo vya elimu, ukosefu wa uzoefu wa kiuongozi, na ukosefu wa rasimali fedha. Vikwazo hivi vinawaathiri zaidi wanawake kuliko wanaume kwasababu jamii inaamini kuwa mwanaume ndio yuko juu katika nyanja zote za maisha. Kutokana na uchambuzi uliofanyika kuhusu mifumo ya maamuzi iliyopo na taratibu zilizopo ndani ya vyama vya siasa kuhusiana na uteuzi wa wagombea, wanawake wanaendelea kutengwa na mifumo isiyojali usawa wa kijinsia – na hivyo kuwaweka wanawake katika hali ya kukata tamaa kushiriki katika harakati za kugombea nafasi za kisiasa. Ili tuweze kuwapata wagombea wanawake na kuwafanya wachaguliwe kwenye majimbo ya uchaguzi, ni muhimu kwa vyama vya siasa kutengeneza mfumo rafiki wa kuteua wagombea utakaozingatia usawa wa kijinsia kwa kuweka kanuni za wazi au kugombea kwa njia zisizo na vikwazo au kuwa na mgawanyo wa nafasi za uongozi kwa kuzingatia jinsia. Mbali ya kuwa na programu za kuwajengea uwezo wanawake, vyama vya siasa vione upo umuhimu wa kufanya marekebisho ya mifumo yake ya ndani na taratibu za kuwapata wagombea kwani hivyo ndivyo vikwazo vikuu kwa wanawake kushindwa kushiriki katika siasa za ndani ya nchi. Sambamba na hilo, sheria za nchi na taasisi inabidi zifanyiwe maboresho ili kuweza kuvilazimisha vyama vya siasa kuzingatia sheria za usawa wa kijinsia na demokrasia. Mapendekezo zaidi kuhusu hatua za kuchukuliwa yatatolewa kwenye muhtasari wa mapendekezo ya kisera unaotokana na utafiti huu.

[50] Mchakato kuhodhiwa na viongozi wa kitaifa maana yake ni kuwa taratibu za kuwateua wagombea haziko wazi kwa wanachama wengi na hakuna kanuni zinazoeleweka kwa wanachama zinazosimamia usawa wa kijinsia kwenye mchakato wa uchaguzi ndani ya chama.

# Marejeleo


ACT [Alliance for Change and Transparency]. (2015). "The Constitution of ACT-Wazalendo";

ACT-Wazalendo, Dar es Salaam.

Anyango, B. O., Alupo, B. A. & Opoku, M. P. (2018). Women in Politics in Kenya: an Analysis of Participation and Barriers. ***Multidisciplinary Journal of Gender Studies,*** 7(1), 1505-1530.

Bratton M and Van de Walle N (1997) ***Democratic Experiments in Africa: Regime Transitions in Comparative Perspective.*** Cambridge: Cambridge University Press.

Brechenmacher, S & Hubbard, C. (2020). Breaking the Cycle of Gender Exclusion in Political Party Development, Working paper. Carnegie Endowment for International Peace.

CCM [Chama cha Mapinduzi]. (1977 [2017]). "The Constitution of Chama cha Mapinduzi"; CCM, Dodoma.

CCM. (2010). "Elections Regulations for Chama cha Mapinduzi"; CCM National Executive Committee, Dodoma.

CHADEMA [Chama cha Demokrasia na Maendeleo]. (2006 [2019]). "The Constitution of CHADEMA"; CHADEMA, Dar es Salaam.

Duverger M (1954) ***Political Parties: Their organisation and activity in the modern state***. London: Methuen.

Edgell, A. (2018). "Vying for a Man Seat: Gender Quotas and Sustainable Representation in Africa" ***African Studies Review, Volume 61, Number 1 pp. 185–214.***

Federation of Women Lawyers in Kenya (FIDA) (2018). A gender analysis of the 2017 general elections in Kenya.

Gallagher M and Marsh M. (1988). ***Candidate selection in Comparative perspective: The secret garden of politics***. London: Sage Publication ltd.

Gauja A and Cross W. (2015). "The Influence of Party Candidate Selection Methods on Candidate Diversity", J***ournal of Representative Democracy Volume 51, 2015 - Issue 3.***

Guariso, A, Ingelaere, B. & Verpoorten, M. (2017). Female political representation in the aftermath of ethnic violence: A comparative analysis of Burundi and Rwanda. WIDER Working Paper 2017/14. United Nations University-WIDER.

Hazan R and Rahat GW (2010) ***Democracy within Parties: Candidate selection methods and their political consequences. Cambridge***: Cambridge University Press.

IFES [International Foundation for Electoral Systems]. (2017). Elections in Senegal: 2017 Parliamentary Elections, Frequently Asked Questions. Arlington: IFES.

Illesanmi, O. O. (2018). Women's Visibility in Decision Making Processes in Africa: Progress, Challenges, and Way Forward. ***Frontiers in Sociology,*** 3 (38), 1-7.

Independent Electoral Commission (IEC South Africa). (2014). National and Provincial Elections of 2014 Report. IEC South Africa.

International IDEA [Institute for Democracy and Electoral Assistance]. (2005). Women in Parliament: Beyond Numbers, A Revised Edition. Stockholm: International IDEA.

International IDEA. (2014). Funding of Political Parties and Election Campaigns: A Handbook on Political Finance. Stockholm: International IDEA.

Levitsky, S and Way, L. A. (2010). Why Democracy Needs a Level Playing Field,

***Journal of Democracy***, 21 (1): 57-68.

Lohmann, A. (2019). Who Really Legislates? The Political Economy of Parliaments in Sub-Saharan Africa. Friedrich-Ebert Stiftung (FES).

Makulilo, A. B. (2014). Baseline Survey for Nomination of Women, Youth and People with Disabilities (PWDs). Tanzania Centre for Democracy.

Makulio, A. B. (2009). "Whose affirmative action is affirmative: Lessons from Tanzania, ***Central European Political Science Journal,*** 4(4): 607-637).

Meena, R. & Makulilo, A. B. (2015). Kanuni za Vyama Vya Siasa za Uteuzi wa Wagombea Kuingia katika Vyombo Vya Maamuzi. Tanzania Centre for Democracy.

National Electoral Commission. (NEC). (1995) Report of the National Electoral Commission on the 1995 Presidential, Parliamentary and Councillors' Elections. Dar es Salaam: Government Printer.

National Electoral Commission. (NEC). (2001) Report of the National Electoral Commission on the 2000 Presidential, Parliamentary and Councillors' Elections. Dar es Salaam: Government Printer.

National Electoral Commission (NEC). (2006) Report of the National Electoral Commission on the 2005 Presidential, Parliamentary and Councillors' Elections. Dar es Salaam: Government Printer.

National Electoral Commission. (NEC). (2011) Report of the National Electoral Commission on the 2010 Presidential, Parliamentary and Councillors' Elections. Dar es Salaam: Government Printer.

National Electoral Commission. (NEC). (2016) Report of the National Electoral Commission on the 2015 Presidential, Parliamentary and Councillors' Elections. Dar es Salaam: Government Printer.

NDI (National Democratic Institute for International Affairs) & UNDP (United Nations Development Programme). (2012). Empowering Women for Stronger Political Parties: A Guidebook to Promote Women's Political Participation.

Norris, P. (2006). The Impact of Electoral Reform on Women's Representation. Acta Politica, 1-17.

Nyaondo, R. A. (2015). Women's Political Representation and Development: The Case of Kenya. *International Journal of Arts & Sciences,* 8(3): 469-482.

Raphael, C. (2010). *Political party institutionalisation in Tanzania: A state project?* MA Diss., University of Dar es Salaam.

Shayo, R. (2005). Women Participation in Party Politics during the Multiparty Era in Africa: The Case of Tanzania. EISA Occasional Paper No. 34 (July). EISA.

Stockemer, D. (2011). Women's Parliamentary Representation in Africa: The Impact of Democracy and Corruption on the Number of Female Deputies in National Parliaments, Political Studies, 59: (693–712).

Sulley C. R. (2015a). The State of Intra Party Politics in Tanzania in Mukandala R.S. The Political Economy of Change in Tanzania: Contestations over identity, the constitution and resources. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Sulley C. R. (2015b). *Opposition political parties in Africa: Kenya and Tanzania in comparative perspective.* PhD Thesis, University of Leipzig, Germany.

TEMCO [Tanzania Election Monitoring Committee]. (1997). The 1995 Elections in Tanzania: Report of the Tanzania Election Monitoring Committee; Dar es Salaam, TEMCO.

TEMCO [Tanzania Election Monitoring Committee]. (2001). The 2000 Elections in Tanzania: Report of the Tanzania Election Monitoring Committee; Dar es Salaam, TEMCO.

TEMCO [Tanzania Election Monitoring Committee]. (2006). The 2005 Elections in Tanzania: Report of the Tanzania Election Monitoring Committee; Dar es Salaam, TEMCO.

TEMCO [Tanzania Election Monitoring Committee]. (2011). The 2010 Elections in Tanzania: Report of the Tanzania Election Monitoring Committee; Dar es Salaam, TEMCO.

TEMCO. (2016). The 2015 Elections in Tanzania: Report of the Tanzania Election Monitoring Committee; Dar es Salaam, TEMCO.

URT [United Republic of Tanzania]. (1977). "The Constitution of the United Republic of Tanzania", Government Printer, Dar es Salaam, Tanzania.

URT. (2019). "The Political Parties Act, 1992 [The Political Parties (Amendments) Act, 2019]".

Von Berge B and and Poguntke T. (2017). in Scarrow S et al 9eds) *Organising*

*Political parties: Representation, participation and power.* Oxford: Oxford University Press.

Zanzibar. (1984). "The Constitution of Zanzibar", Government Printer, Zanzibar, Tanzania.

## KIAMBATISHO NA. 1: WATU WALIOSHIRIKI

| S/N | JINA | CHEO | ANAKOTOKA (CHAMA AU SHIRIKA) |
|---|---|---|---|
| 1 | Dorothy Semu | Makamu Mwenyekiti (Bara) | ACTWazalendo |
| 2 | Savelina Silvanus Mwijage | Mjumbe wa Hakamshauri Kuu Taifa, ACT-Wazalendo & Mbunge wa zamani wa Viti Maalumu, CUF | ACTWazalendo |
| 3 | Mwanaharusi Bunduki | Naibu Katibu Mkuu (Wanawake) | ACTWazalendo |
| 4 | Shani Khalfan Beleko | Mgombea wa zamani wa Udiwani na mtia nia wa Udiwani mwaka 2020 | ACTWazalendo |
| 5 | Dkt. Bashiru Ally Kakurwa | Katibu Mkuu | CCM |
| 6 | Queen M. Mlozi | Katibu Mkuu, UWT | CCM |
| 7 | John Mnyika | Katibu Mkuu | CHADEMA |
| 8 | Reginald Munisi | Mkurugenzi wa Uchaguzi na Uratibu | CHADEMA |
| 9 | Tumaini Makene | Mkuu wa Habari wa Mawasiliano | CHADEMA |
| 10 | Elizabeth Masanja | Mratibu, BAWACHA | CHADEMA |
| 11 | Anatropia Theonest | Mbunge wa Viti Maalumu na aliyewahi kugombea Ubunge Jimbo la Segerea | CHADEMA |
| 12 | Martha Mtio | Diwani, Kawe | CHADEMA |
| 13 | Magdalena Sakaya | Naibu Katibu Mkuu na aliyewahi kuwa Mbunge | CUF |
| 14 | Anna Paul Ryoba | Katibu Mtendaji, Wanawake | CUF |
| 15 | Yusuph Mohamed Mbungiro | Utawala na Uratibu | CUF |
| 16 | Martin Bernard Mung'ong'o | Mkuu wa Uchaguzi na Kampeni | NCCRMageuzi |
| 17 | Ester Corneli Komba | Naibu Katibu Mkuu, Wanawake | NCCRMageuzi |
| 18 | Sisty Nyahoza | Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa | ORPP |
| 19 | Fausta Mahenge | Mwanasheria wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi | NEC |
| 20 | Said Wamba | Naibu Katibu Mkuu | TUCTA |
| 21 | Fatma Amani Karume | Wakili wa Mahakama Kuu na IMMMA Advocates | IMMMA Advocates |
| 22 | Daniel Loya | Mkurugenzi Mkuu, Kituo cha Demokrasia Tanzania | TCD |